

Mtu anapozaliwa lazima apitie hatua kadhaa ili kukamilisha hatua zake za ukuaji, pia mtu huyu akiruka hatua moja hatakuwa na ukamilifu wote wakuitwa kwajina la mtu mzima aliye kusudiwa. Utaona akipewa majina mbalimbali kutokana na muonekano tofauti na wenzako. Na hili ndilo jambo kuu ambalo limenipa msukumo mkubwa kuandaa somo hili kwa lengo la kuliponya kanisa la leo katika ulimwengu wa ukengefu. Pia somo hili lita msaidia mkristo kujua maisha ya kila mwamini kuwa yupo katika hatua gani ili ajue kumpatia chakula sitahiki kulingana na hatua aliyo nayo mwamini huyo. Watumishi wengi hasa huduma ya ualimu katika huduma kuu tano za kulijenga kanisa imeleta matatizo mengi kanisani hasa ikiwemo kufukuza baadhi ya washirika na wengine kuhamahama makanisa na wengine kurudia dhambini kutokana na udhaifu wa mafundisho yanayotolewa na mwalimu husika. Sio kwamba mwalimu anafundisha mambo tofauti na biblia inavyosema hapana ila anayefundishwa ni nani, na ana umri gani, je hatua aliyo nayo inamruhusu kujifunza somo hilo? msomaji wangu wa somo hili utaweza kujifunza mambo mengi katika pamfleti hii ambayo yatakusaidia wewe kutoa mafundisho bora kwa watu wa Mungu kulinga na viwango vyao vya kupokea ili wafike mbinguni ambako ndio kusudio la wengi. Usipange kuishia njiani wakati wa kusoma kila ukurasa umebeba ujumbe mzito wa kukutoa wewe kama mkristo mahali Fulani.